JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

AGOSTI 2023

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA NANE




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA

www.pmo.go.tz

## Waziri Mhagama, Ahimiza kuwepo muongozo na mfumo wa ufuatiliaji na utendaji wa shughuli za serikali

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama, Ameitaka Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali, kuharakisha kutengeneza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Utendaji wa Shughuli za Serikali Pamoja na kukamilisha na kuzindua haraka Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ndani ya nchi utakaotumika na Seriali kwa ujumla, Wizara, Taasisi na maeneo yote ya Utendaji kazi ndani ya Serikali.

Ameyasema hayo Jijini Arusha, alipofungua Mkutano wa Mazingativu uliyohusisha, Viongozi, watumishi wa Ofisi hiyo Pamoja na Taasisi zake.

Sambamba na hilo, Pamoja na kuonesha Imani wa Mkurugenzi wa Idara hiyo mpya, Waziri Mhagama aliitaka pia idara hiyo kuwa na Ubunifu

"Jaribuni kununua mifumo, miundo na taratibu za kufanya ufuatiliaji na Tathmini kutoka kwenye mataifa mengine, ili tuweze kuitangaza Taifa letu kwa kazi hili kuwa tunaweza kufanya vizuri" Alisisitiza Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama alisema anahitaji kupata taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Ofisi yake na Serikali kwa ujumla wa kila robo mwaka ikiwa ni katika kuboresha Eneo hilo.

Akizungumzia kuhusu Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali, Waziri Mhagama alisema katika eneo hilo, katika mwaka huu Mpya wa Fedha 2023/2034, Serikali imejiwekea mkakati wa kuongeza Maduhuli na mapato ya yake kupitia Mpigachapa Mkuu wa Serikali, ambapo ujenzi wa Mradi wa Mkakati wa kiwanda kipya cha Mpigachapa Mkuu wa Serikali Umefikia asilimia 97%

"Tumeshaanza kufanya manunuzi ya mashine za kisasa, na tumeshafufua mashine ambazo zilikuwa zimeharibika.

Nisisitize Chapa muendeshe kiwanda kwa Ubunifu, jengeni fikra mpya boresheni mifumo miundo na namna ya uhifadhi na uchapaji wa nyaraka za Serikali, nataraji kiwanda hiki kinaweza kikajiuza na kinaweza kikapata soko la nchi za kusini mwa Afrika SADC na katika na Soko la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, pale mnalo jambo na kazi kubwa ya kufanya, na mazingativu haya yawasaidie kujiongoza na kupata picha na fikra ambazo zitatuvusha." Alisisitiza Waziri Mhagama

Akiongea katika Mkutano huo wa Mazingativu, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Dkt Jim Yonazi alisema kuwepo kwa Ofisi hiyo Jijini Arusha katika Mkutano huo ni kutokana na nia ya Ofisi hiyo kuhakikisha kwamba inatenda majukumu yake kwa umakini na kwa utimilifu ikiwa ni pamoja na Uratibu wa shughuli za Serikali kwa ujumla na kwenye maeneo mengine.



"Tunaweza kujifunza kutoka hapa ndani ya nchi mambo mengi na tukatumia ubunifu na wataalam wa ndani katika utendaji na hakuna mtu anaweza kuwa mbunifu katika mazingira yenye stress, hivyo tunaweza kuweka mazingira wezeshi kwa watumishi na kukuza na kuongeza uelewa katika utendaji."Alisema

.



Waziri Mhagama, Ahimiza mashirikiano

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu ) Mhe. Jenista Mhagama ameitaka Idara ya Ufutiliaji na Tathimini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini, (TAKUKURU) katika kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathimini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali, ili kuweza kuondoa upendeleo, Rushwa na kutoa huduma bora kwa wananchi katika utendaji Serikalini.

Kauli hiyo ameitoa leo Jijini Dodoma alipokuwa katika kikao kazi cha Mapitio kilichohusisha Wakurugenzi, wa Idara na Wakuu wa vitengo wa Ofisi hiyo ambapo, imefanya wasilisho la Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa shughuli za Serikali.

Waziri Mhagama Alisema kuwa, eneo la Ufuatiliaji na Tathmini ni eneo ambalo haliwezi kukwepeka "Leo Tumekutana hapa tumefanya kazi nzuri ya kufanya mapitio na kuangalia ramani hii ambayo inaanza na kuwa na mfumo wa Ufuatilia na Tathmini Nchini, kama nyenzo muhimu sana ya Utendaji kazi ndani ya Serikali." Alisisitiza

Aliendelea kusema kuwa, Mfumo huu utasaidia kushauri namna ya kujipanga na namna ya kufanya kazi ndani ya Serikali,

"Mfumo huu utusaidie kuchakata kila kitu na kutusaidia kupata matokeo sahihi kwa jambo sahihi na shughuli sahihi, katika kupima utendaji kazi na matokeo yake." Alifafanua.

Aidha, Alisema pia kwa Mujibu wa Sheria kuna Taasisi ambazo zimekasimiwa majukumu ya kufanya, zinazofanana na Idara hii akitolea mfano Tume ya Taifa ya Mipango, na kusema ni lazima kukutana na Tume hii ya Mipango ili kila mtu afanye kazi kwa kufuata Sheria na Kuzingatia Mifumo iliyopo. "Ni lazima kufanya Tathmini na Ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya fedha katika Utekelezaji wa Miradi na utendaji wa shughuli za Serikali, eneo hili kwenye mfumo liwekwe vizuri na liweze kutusaidia," Alisema. Kwa Upande wake Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga, Alisema Mamlaka ya Serikali Mtandao (Ega) imefanya wasilisho zuri lenye kutoa muelekeo wa Utendaji wa Shughuli za Serikali Utakaosaidia Ofisi ya Waziri Mukuu kuratibu vizuri shughuli za utendaji Serikalini .



# Naibu Waziri Ummy, Atoa wito kwa wananchi kutembelea vivutio vya utalii

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia na (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga ametoa rai kwa wananchi, Taasisi na Wizara kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kutembelea vivutio vyetu vya utalii wa ndani.

Wito huo umetolewa wakati Viongozi na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, walipotembelea Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro baada ya kutoka katika Mkutano wa Mazingativu Mkoani Arusha.

"Tunamshukuru na kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi kubwa alizozifanya katika sekta ya utalii kupitia filamu ya Royal tour," alibainisha.

"Tumefika Ngorongoro na tumejionea wageni wamefurika wamekuja kujionea vivutio vya utalii." Alisisitiza.

Aidha, alitoa shukrani nyingi Kwa Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa kwa kutoa ruhusa ya kutembelea eneo hilo la Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro.

Aliongeza Kwa kusema kuwa, ziara hiyo imeimarisha upendo, uongozi na urafiki kati ya viongozi na watumishi na itaongeza hari ya utendaji kazi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia na (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim Yonazi amesema, ziara hiyo ni Maelekezo ya Mhe. Waziri Mkuu kwa lengo la kuhakikisha kwamba tuna viongozi wa kusimamia Sera na wanalifahamu eneo la utalii wanaloliratibu Sera zake katika Serikali.




Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia na (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga akiwa katika picha na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulika na (Sera Bunge na Uratibu) Dkt. Jim Yonazi na Naibu Katibu Mkuu Bwn. Anderson Mutatembwa alipotembelea Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro.

## Dkt. Yonazi: Sekta ya kilimo kuchagiza pato la Taifa

Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini kwa kuzingatia umuhimu na tija ya sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi wakati akihutubia katika kikao cha Awali cha Wadau kwa ajili ya zoezi la Tathmini ya Nusu Muhula na Uandaaji Mpango wa Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) kwa miaka mingine mitano kilichofanyika Jijini Dar es salaam.

Dkt. Yonazi alieleza kuwa sekta ya kilimo ni muhimu kwa Taifa na tegemeo kwa maisha ya wananchi wengi kwani huongoza inaongoza kwa uchangiaji mkubwa katika pato la Taifa, na robo tatu ya bidhaa zinazouzwa nje ya Nchi.

Aliongeza kuwa sekta ya kilimo imeendelea kuwa chanzo cha chakula pamoja na utoaji wa fursa za ajira zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania ambapo katika mwaka 2021, sekta hiyo ilichangia asilimia 26.1 katika shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa.

Alifafanua kuwa, kilimo kimekuwa na uhusiano na sekta zisizo za kilimo kupitia usafirishaji kwenda kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi na uuzaji nje ya nchi pamoja na malighafi kwa viwanda na masoko kwa bidhaa zilizotengenezwa akieleza kuwa hatua hiyo imechagiza ongezeko la bajeti kubwa katika sekta ya kilimo kwa miaka miwili mfululizo.

Aidha alitumia fursa hiyo kuwapongeza wadau mbalimbali wanaoendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuyafikia malengo yake ikiwemo Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO).

“Nichukue fursa kulishukuru Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) kwa kuunga mkono juhudi hizi ambapo wamewezesha kwa kujengea uwezo timu ya wataalam wa ndani itakayoshirikiana na Mshauri Elekezi katika zoezi hili. Timu hiyo itakuwa na mchango mkubwa katika kutoa taarifa na maoni ambayo yatazingatiwa na Mshauri Elekezi kabla ya vikao vya wataalam na viongozi,”alisema Dkt. Yonazi.



Aidha, alishukuru ushiriki wa Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu wataalam wao kushiriki katika kikao hicho muhimu kwa sekta ya kilimo.




Mwongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera za Kisekta, Zanzibar – 2022 wazinduliwa

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) Mhe.Hamza Hassan Juma amezindua Mwongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera za Kisekta, Zanzibar – katika Ukumbi wa Shekh Idrissa Abdul - Wakili Kikwajuni Zanzibar.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo amesemea kuwa ni miongoni mwa muendelezo wa utekelezaji wa hati ya kisheria Nambari 14 ya mwaka 2020 iliyoitaka ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kupitia Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo kusimamia

Mhe. Hamza alisema, Ofisi yake imechukua jitihada mbali mbali za kuifanyia kazi hati hiyo ya kisheria ikiwemo kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Sera za Serikali ambapo tathmini ya kina kwa Sera 39 ilifanyika na mambo mbalimbali yalibainika yakiwemo mapungufu, mafanikio na changamoto zilizopo katika kusimamia uratibu wa uandaaji na utekelezaji wa Sera nchini.

"Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kutokulingana kwa miundo ya kisera nchini jambo ambalo linaweza kurejesha nyuma upatikanaji halisi wa utekelezaji wa Sera.Aidha, kupitia Ripoti ya Tathmini hiyo pamoja na mambo mengine Ofisi yangu imeandaa Mwongozo huu ambao utakuwa umetatua changamoto mbali mbali na utaleta matarajio mazuri katika uratibu wa Sera nchini kwa maslahi ya nchi yetu," alisema Mhe. Hamza

Aliongezea kuwa Mwongozo umezingatia miongozo ya Kikanda na Kimataifa, Ilani ya Uchaguzi 2020 – 2025 na Mipango ya Maendeleo Endelevu ya Kitaifa na Kimataifa.

"Ofisi inaimani kikao hichi chenye ushiriki wa Makatibu wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Mashirika, Wakurugenzi, Wakuu wa Vyuo, Sekta Binafsi na Maafisa Viungo wanaosimamia Sera ni ishara njema inayoonesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyojali ushirikishwaji wa Taasisi za Umma na za Binafsi katika kusimamia maendeleo ya nchi hii," alieleza.

Aidha, uzinduzi ulihusisha wajumbe kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni ishara na kielelezo cha Muungano wetu kuhakikisha inaendeleza mashirikiano hasa katika Sera zinazotekelezwa katika pande zote mbili za Muungano kwa kuwa na mikakati ya pamoja ya utekelezaji wa Sera zenye sura ya Muungano.

Alitoa wito kwa Wizara zote kutoa elimu stahiki ya Sera zao na kuandaa utaratibu wa ushirikishwaji wa wadau husika katika uandaaji na utekelezaji wa Sera hizo sambamba na kuufanyia kazi mwongozo huu kwa manufaa ya umma.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz